HISTORIA YA MCHAKATO WA KUTANGAZWA MTAKATIFU
SISTA MARIA CAROLA CECCHIN, MSTAHILI-HESHIMA

Mchakato wa Kikanuni unaotangulia tangazo la mtakatifu mpya ni safari ndefu sana na inajumuisha awamu mbili, awamu ya kijimbo, na awamu ya Kirumi.

Awamu ya Kijimbo hufanyika katika ngazi ya jimbo na ni jukumu la Askofu Mahalia wa eneo alipofia mkandidati wa machakato kuchunguza kwa kina Ushahidi kuhusu Maisha yake, kiwango cha fadhila zake, umaarufu wa utakatifu wake, maandishi yake and miujiza aliyoifanya mwenyewe au iliyotokea kwa njia ya maombezi yake. Baada ya uchunguzi hii wa kwanza na kutangazwa kwake kuwa "mtumishi wa Mungu", askofu mahalia upelekewa rasmi hati za mchakato wa kijimbo huko Roma, katika "Baraza la Kipapa la Mchakato wa kuwatangaza Watakatifu"

Uchunguzi wa kijimbo katika mchakato wa Mtumishi wa Mungu Sista Maria Carola ilifunguliwa miaka 89 baada ya **kifo chake, mnamo Aprili 24, 2014**, katika Jimbo Kuu la Torino, na Askofu Mkuu Mons. Cesare Nosiglia na kuhitimishwa katika kanisa la Chumba Kidogo ya Mungu Mpaji huko Torino mnamo **Oktoba 7, 2014,** mbele ya Askofu Mkuu mwenyewe, baada ya vikao 17 vya uchunguzi.

Kwa nini baada ya miaka mingi kiasi hicho? Sababu ya kucheleweshwa kias hicho ingeonekana kuwa rahisi kwa sababu ilifuatia mafundisho ya Mwazilishi Mt. Joseph Benedict Cottolengo ambaye hakutaka wanawe na mabinti zake watafute utakatifu wa kufikia madhabahuni bali ushujaa wa maisha ya kila siku ya utakatifu na kusherehekea *baada ya kifo* huko mbinguni.

Haikuwa hivyo kwa Sista Maria Carola. Mwaka mmoja baada ya kifo chake, sista mwenzake Scolastica Piano, naye pia mmsionari Africa hadi mwaka 1919, aliona umuhimu wa kukusanya ushuhuda kutoka kwa masista wamisionari, Mapadre wa Consolata, Mabruda na watu waliomfahamu mtumishi wa Mungu na kuchapisha wasifu wake katika kitabu chenye jina "*Soavi memorie di Suor Maria Carola, Vincenzina del Beato Cottolengo nella Piccola Casa della Divina Provvidenza in Torino"*. Bila shaka kitabu hiki, pamoja na mapungufu ya wasifu za wakati huo kuwa na mwelekeo wa kusambaza taarifa nzuri tu, ni chemchemi muhimu na ya kutegemewa katika kupata taarifa za maisha ya Mtumishi wa Mungu.

Ikumbukwe kuwa taarifa zilitajwa humo ndani zimedhibitishwa na utafiti na uchunguzi wa kina uliofanya na wanahistoria wa Mapadri wamissionari wa

Suor Lucia Mossucca - Stefano Di Lullo
www.cottolengo.org
Via Cottolengo, 12 - 10152 Torino, cell. +39 345 6216561
ufficiostampacottolengo@cottolengo.org

Consolata wakiwemo: Candido Bona, Alberto Trevisiol, Igino Tubaldo; kama vile katika nyaraka kwenye Hifadhi-nyaraka muhimu: Nyaraka za Siri za Vatikani, Nyaraka za Kihistoria za Propaganda Fide, Nyaraka za Taasisi ya Umisionari ya Consolata na Nyaraka za Shirika la Masista wa Cottolengo.

Uchambuzi uliofanyika unaonyesha kuwa umaarufu wa utakatifu wake haukuwahi kupungua; tayari ulikuwa hai wakati wa miaka ya mwisho ya utume wake huko *Meru* (Kenya) umekuwa kiongezeka zaidi na zaidi baada ya kifo na katika miaka iliyofuata, hadi leo nchini Italia, na zaidi ya yote barani Afrika.

b) Katika awamu ya Kirumi ya Mchakato, padre aliyeteulia na Baraza la Kipapa, baada ya kusoma kwa makini hati, huandaa ripoti na kuiwailisha kwa makardinali ambao ndio wanaounda Baraza lenyewe. Baada ya kuidhinishwa na Baraza, Papa, kwa kutambua ushujaa wa fadhila zake Mtumishi wa Mungu, humtangaza “Mstahili-Heshima”.

Mchakato wa Sr. Maria Carola Cecchin katika ngazi ya Kirumi ulikuwa na Mons. Maurizio Tagliaferri kama Relator na Sista Antonietta Bosetti (Mtawa wa Mt. Joseph Benedict Cottolengo) kama postulator, na ulipata idhini kisheria mnamo **Mei 29, 2015**.

Baada ya kuwasilisha *mkusanyiko wa nyaraka (positio), muhimu* kwa wanahistoria na wanateolojia kuchunguza maisha ya Mtumishi wa Mungu **Oktoba 10, 2017** maamuzi ya uthibitisho wa wanahistoria juu yake yalitolewa na **mnamo Februari 4, 2020** ya wanateolojia walitoa maamuzi yake chanya. Mnamo **Novemba 10, 2020** palikuwa na maoni ya kupendeza zaidi ya Mkutano wa Kawaida wa Makardinali na Maaskofu.

Mnamo Novemba **23, 2020**, baada ya kusikia Rais wa Baraza la Kipapa kuhusu Mchakato wa kutangazwa Watakatifu Kardinale mteule Mons. Marcello Semeraro, Papa wake Papa Francis aliidhinisha uchapiswaji wa hati kuhusu fadhila za kishujaa za Mtumishi wa Mungu, akimtangaza Mstahili-heshima.

Ni hatua gani zifuatazo?

Katika uthibitisho wa tukio la muujiza wa kwanza kwa njia ya maombezi ya mstahili-heshima mpya, Papa angeweza kumtangaza "mwenyeheri".

Katika kesi ya Sista Maria Carola, tukio linalodaiwa kuwa la kimiujiza lisilo na maelezo kisayansi limeshatokea na kuwasilishwa, kukubaliwa na kuchunguzwa na wataalam wa Baraza la kipapa la mchakato wa Kuwatangaza Watakatifu, huku wakisubiri atangazwe “Mstahili-heshima”. Sasa tutalazimika kuendelea na

Suor Lucia Mossucca - Stefano Di Lullo
www.cottolengo.org
Via Cottolengo, 12 - 10152 Torino, cell. +39 345 6216561
ufficiostampacottolengo@cottolengo.org

uchambuzi, majadiliano na kulinganisha matokeo na kufikia maamuzi ya kutamka kwa uhakika muhuri wa Mungu juu ya utakatifu wa huyu sista.

Baada ya muujiza wa pili, Papa atamtangaza mwenyeheri kuwa "mtakatifu", hivyo kuhitimisha mchakato wa kikanoni. Katika hatua hii, mtakatifu mpya ataorodheshwa katika "kanuni" rasmi (= orodha) ya watakatifu waliotukuzwa na Kanisa na tarehe ya sikukuu yake ya kiliturujia itawekwa. Tarehe hii inaendana na siku ya kifo cha mtakatifu, inayozingatiwa kama siku ya kuzaliwa katika uzima wa milele.

Ni matumaini yetu kwamba Sr Maria Carola hivi karibuni atakuwa mwenyeheri mpya katika kanisa hasa kwa sababu barani Afrika kumbukumbu yake bado iko hai!

DEO GRATIAS!

Suor Lucia Mossucca - Stefano Di Lullo
www.cottolengo.org
Via Cottolengo, 12 - 10152 Torino, cell. +39 345 6216561
ufficiostampacottolengo@cottolengo.org